



BARAZA LA DIASPORA LA WATANZANIA DUNIANI
Tanzania Global Diaspora Council

TAARIFA KWA DIASPORA

Baraza la Diaspora la Watanzania Duniani (TDC Global) linawajulisha watanzania wote waishio ughaibuni kuwa Mhe. Balozi Dkt. Willibrod Peter Slaa, Balozi wa Nodiki, Baltiki na Ukraine ambaye pia ni Mlezi wa TDC Global amemaliza muda wake wa utendaji katika ubalozi wetu wa Tanzania nchini Uswidi. Kwa hiyo, tunategemea kumpokea balozi mpya katika siku za karibuni.

Mwenyekiti wa TDC Global Bi. Bupe Amon Kyelu anapenda kuwafahamisha kuwa TDC Global inategemea kupata mlezi mpya. Yatokanayo na kikao cha Kamati Kuu ya TDC Global cha tarehe 3 Augusti 2021, kikao kilikubaliana kufanyika kwa mkutano kupitia mtandao wa Zoom ambao utakuwa wa kumuaga mlezi wetu Mhe. Balozi Dkt. Willibrod Peter Slaa. Mkutano huo utawashirikisha vyama na diaspora wote watanzania Duniani.

Mkutano utafanyika jumamosi tarehe 4, Septemba 2021, kuanzia saa saba mchana (13:00) hadi saa tisa mchana (15:00) - saa za Tanzania. Tafadhali zingatia muda kulingana na muda wa nchi yako ya makazi.

Diaspora wote mnaombwa kushiriki kwa pamoja kusikiliza nasaha za mlezi wa TDC Global kwa mara ya mwisho akiwa katika nafasi hiyo. Ratiba na taarifa nyingine za kushiriki katika mkutano huo zitatolewa kwa kadri zinavyokamilika. Taarifa zitapatikana pia katika tovuti yetu ya TDC Global WWW.TDCGLOBAL.ORG

Diaspora na Nyumbani

Agnes Lerdorf

Mwenyekiti

Mahusiano ya Umma

Agosti 15, 2021

